**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**610** **UALIMU**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka: 2000**

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B**, **C, D** na **E.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na swali **moja (1)** kutoka katika kila sehemu **B**, **C, D** na **E.**
3. Sehemu A ina alama 40, sehemu B, C, D na E zina alama 15 kila moja.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza maana ya Saikolojia ya Elimu na fafanua umuhimu wake kwa kazi ya ualimu.
2. Bainisha kwa maelezo namna mazingira ya shule yanavyoweza kuathiri ujifunzaji wa mwanafunzi.
3. Eleza sababu nne zinazoonyesha umuhimu wa mbinu shirikishi katika ufundishaji.
4. Orodhesha na eleza aina nne za mitihani kulingana na madhumuni yake.
5. Eleza athari chanya za mawasiliano bora kati ya mwalimu na mwanafunzi.
6. Eleza tofauti kati ya motisha ya ndani na motisha ya nje kwa mifano.
7. Andika faida tatu za kutumia vifaa vya kufundishia darasani.
8. Eleza changamoto tatu zinazojitokeza wakati wa upimaji wa wanafunzi.
9. Eleza maana ya tathmini endelevu na umuhimu wake.
10. Eleza umuhimu wa nidhamu katika uendeshaji wa shule.

**SEHEMU B: SAIKOLOJIA YA ELIMU (Alama 15)**

Jibu swali **moja (1)** tu katika sehemu hii.

11. Mwalimu wa Darasa la Tano anagundua kuwa wanafunzi wake wengi wanashindwa kuelewa dhana za kihisabati zinazohusisha vitu dhahania. Kwa kutumia nadharia ya Jean Piaget, eleza sababu za hali hiyo na mapendekezo ya kielimu yanayofaa.
12. Katika shule moja ya sekondari, wanafunzi wawili wenye uwezo sawa huonesha tofauti kubwa katika ufaulu. Jadili hali hiyo kwa kuzingatia mchango wa urithi na mazingira katika ujifunzaji.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU C: MITAALA NA UFUNDISHAJI (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** tu katika sehemu hii.

13. Serikali imeanzisha marekebisho ya mtaala ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira. Eleza maana ya mtaala na jadili vipengele vyake muhimu katika muktadha wa mabadiliko hayo.

14. Mwalimu mpya ameajiriwa shuleni lakini anakosa ufanisi darasani. Kwa kutumia nadharia za ufundishaji, eleza mbinu tatu ambazo zingemsaidia kuboresha ufundishaji wake.

## SEHEMU D: UTAFITI WA KIELIMU, UPIMAJI NA TATHMINI (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** tu katika sehemu hii.

15. Mkuu wa shule anataka kujua sababu za kushuka kwa ufaulu wa wanafunzi wake. Eleza hatua kuu za utafiti wa kielimu anazoweza kufuata ili kupata majibu ya tatizo hilo.

16. Katika mitihani ya mwisho wa mwaka, matokeo ya darasa moja yanaonekana kutokidhi uhalisia wa uwezo wa wanafunzi. Jadili umuhimu wa uaminifu na uhalali wa vipimo katika hali hiyo.

## SEHEMU E: MISINGI YA ELIMU (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** tu katika sehemu hii.

17. Jamii fulani inaamini kuwa elimu haina mchango mkubwa katika maendeleo. Kwa hoja za kielimu, eleza jinsi elimu inavyoweza kuwa chombo cha maendeleo ya jamii.

18. Tanzania imepitia sera mbalimbali za elimu tangu uhuru. Jadili mchango wa sera hizo katika kuimarisha mfumo wa elimu.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org